

HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2020 HADI MACHI,2020

1.0 UTANGULIZI

Ndugu Wananchi,

Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ni miongoni mwa Mamlaka za Serikali za Mitaa nane zilizopo katika Mkoa wa Tabora. Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 14,050 ambalo ni sawa na asilimia 18.8 ya eneo la Mkoa wa Tabora. Kiutawala Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ina jumla ya Kata 28, Vijiji 99 na Vitongoji 458. Kwa mwaka 2019 Wilaya ya Kaliua inakadiriwa kuwa na idadi ya watu 546,157 ambapo kati yao wanaume ni 272,648 na wanawake ni 273,509. Asilimia ya ongezeko la watuni 4.8% kwa mwaka.

Ndugu Wananchi,

Napenda nichukue fursa hii kutoa kwa ufupi taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kwa sekta mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kipindi cha tatu kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2020 HADI MACHI, 2020

Ndugu Wananchi,

Kwa kipindi cha Januari, 2020 hadi Machi, 2020 Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua imeweza kutekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

- 1.Halmashauri kupitia Elimu ya Kujitegemea (EK) imeendelea na ujenzi wa miundombinu katika sekta ya Elimu. Ambapo wanafunzi wameshiriki kikamilifu katika ufyatuaji wa tofari, Halmashauri kuchangia saruji na jamii kuchangia gharama za ufundi na mchanga. Jumla ya vyumba vya madarasa 118 (Shule za Msingi 63 na Sekondari 55) vimejengwa na maboma yamekamilika. Wananchi wanaendelea kuchanga fedha kwa ajili ya maandalizi ya upauaji. Lengo ni kuhakikisha wanafunzi wote wanapata mahali pa kusomea na kujifunzia.

- 2.Pia, Halmashauri imenunua bandali 300 za bati sawa na pc 3600 zenyе thamani ya milioni 80 kwa ajili ya upauaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Bati hizi zitagawiwa katika kata ambazo zimekamilisha maboma na zimekamilisha manunuzi ya mbao na vifaa vyote vinavyohusiana na upauaji.
3. Aidha, Halmashauri imeendelea na ujenzi wa vyumba 6 vya maabara shule za sekondari kanoge, Kamsekwa, Zugimulole Silambo, Seleli na Ilege kupitia mapato ya ndani ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya serikali.
- 4.Tunaishukuru serikali kwa programu ya Elimu bila malipo. Hadi sasa, Halmashauri imepokea jumla ya Tzs 1,083,768,929.97. Mchanganuo wa fedha hii ni kama ifuatavyo; Tzs 683,967,339.63 kwa ajili ya shule za msingi na Tzs 399,801,590.34 shule za sekondari.
- 5.Halmashauri imeendelea na ujenzi wa miundombinu mbaalimbali kupitia mapato ya ndani. Ujenzi wa Vituo vya afya 3 vya Usinge, Mwongozo na Uyowa. Ujenzi wa nyumba ya mtumishi zahanati ya Nsimbo. Ujenzi wa zahanati 3 za Kingwangoko, Usangi na Ichemba zipo hatua ya ukamilishaji na zinatarajiwа kuombewa kibali kwa ajili ya kufunguliwa. Zahanati 5 za Mkuyuni, Usonga, Utantamke, Igombe na Shella (Luganjo mtoni) zimepauliwa. Hii yote ni kuboresha upatikanaji wa huduma ya Afya kwa wananchi. Hivyo, niwaombe sana wananchi muendelee kuchangia ujenzi wa miundo mbinu mengine na Halmashauri ya Wilaya itaendelea kuwaunga mkono ili kuboresha huduma za afya kwa jamii.
- 6.Halmashauri imenunua mifuko 1,683 kutoka kampuni ya saruji ya DANGOTE. Saruji hii ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Elimu na ujenzi wa miundombinu hospitali ya Wilaya. Elimu mifuko 600, Wodi ya watoto 890, na Ujenzi wa duka la dawa la Halmashauri mifuko, 193.

7. Katika kuhakikisha huduma za maji zinasogezwa kwa wananchi na kupunguza adha ya kutembea umbali mrefu. Usambazaji wa Maji ya bomba katika kijiji cha Kazanaupate na Kaliua mjini unaendelea. Pia, maandalizi ya ujenzi wa mradi wa maji ya bomba katika vijiji vya Kanoge, Ichemba, Ushokola, Wachawaseme na Imalampaka yamefanyika na ujenzi utaanza muda wowote. Aidha, ukarabati wa visima virefu15 vya pampu za mikono umefanyika. Kila Mtendaji wa kata na kijiji anajukumu la kulinda mali za uma na kufanya matengenezo madogo madogo pindi yanapotokea badala ya kuripoti kwa Murugenzi.
8. Utoaji wa mikopo umefanyika kwa vikundi vilivyokidhi vigezo katika kata zote. Hadi sasa, jumla ya shs 345,000,000/= zimetolewa kwa mchanganuo ufuatavyo; Sh 133,500,000/= kwa vikundi vya vijana, Sh184,000,000/= kwa vikundi vya Wanawake na shs 27,500,000/= kwa vikundi vya Walemavu. Hivyo, niombe vikundi vilivyokopeshwa kurejesha marejesho yao kwa wakati ili vikundi vingine viweze kupatiwa mikopo. Na wanaodaiwa waendeele kulipa kabla ya kufikishwa Mahakamani kwani TIBA YA DENI NI KULIPA.
9. Katika mwaka 2018/2019 Halmashauri iliandaa hesabu za Fedha za Serikali na kuwasilisha kwa mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kutokana na Hesabu hizo Mkaguzi Mkuu ametoa Hati safi kwa Halmashauri ya Kaliua.
10. Halmashauri inaendelea na jitihada ya kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona ambapo hadi sasa imeshatenga kituo kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa watakaopatikana, imetoa mafunzo kwa watumishi wa Afya na inaendelea kuhamasisha wanaanchi kuzingatia maelekezo ya wataalam wa Afya ikiwa pamoja na kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji yanayotiririka. Aidha, inahimiza wananchi kuvalaa barakoa wanapokuwa kwenye msongamano inapolazimu.

2.1 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MAPATO YA NDANI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua imekisia kukusanya na kutumia mapato kutohana na vyanzo vyake vya ndani yenye jumla ya Shs 3,807,985,935.00. Hadi tarehe 31/03/2020 jumla ya Shs 2,440,281,957.64 zilikuwa zimekusanya sawa na asilimia 64. Nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa madiwani wote, Mkurugenzi Mtendaji na Wataalamu wote kwa ushirikiano mnaouunesha katika suala zima la ukusanyaji wa mapato ya ndani. Aidha, niwaombe ushirikiano uendelee na kasi ya ukusanyaji wa mapato iongezeke ili kupitia mapato hayo tuweze kuboresha huduma kwa jamii.

2.3 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI.

Ndugu Wananchi,

Katika utekelezaji na usimamizi wa shughuli za Halamshauri kwa kipindi cha januari, 2020 hadi Machi, 2019, changamoto kwa ujumla zilizojitokeza ni kama ifuatavyo:-

- 1.Kuchelewa kwa fedha za miradi kutoka Serikali Kuu na wafadhili hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi.
- 2.Upungufu mkubwa wa miundombinu ya kutolea huduma kwa jamii kwa sekta za Afya na Elimu kama vile Vyumba vya madarasa shule za msingi na sekondari,nyumba za walimu na mabweni,chumba cha upasuaji nk.
- 3.Upungufu wa watumishi hususani katika Sekta ya Afya na Watendaji wa vijiji hali inayosababisha kupunguza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

2.4 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Halmashauri imejipanga kufanya yafuatayo:-

- 1.Halmashauri imeweka mkazo katika dhana ya Elimu ya kujitegemea ili kuongeza miundombinu mashulen. Ununuzi wa saruji na ununuzi wa bati kupitia mapato ya ndani imekuwa chachu ya kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu mashulen. Aidha, Halmashauri kupitia

mapato ya ndani itaendelea kuongeza nguvu katika ukamilishaji wa miradi iliyoanzishwa na wananchi ikiwa ni mkakati wa kukabiliana na uhaba wa miundombinu sekta ya Elimu.

- 2.Kuendelea kuhamasisha wananchi juu ya uchangiaji wa ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za jamii kama vile zahanati, vyumba vya madarasa, vyoo, nyumba za walimu na madawati.
- 3.Halmashauri inaendelea kuwasiliana na Tume ya menejimenti ya utumishi ili kupata watumishi wa kada mbalimbali. Lengo ni kupunguza uhaba wa watumishi uliopo,kuboresha utendaji kazi na kuongeza ufanisi kazini.

3.0 HITIMISHO

Ndugu Wananchi,

Ukuaji wa Uchumi na maendeleo ya Kaliua unategemea juhudzi za Wanakaliua wenyewe. Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi hususani katika sekta za Umeme, Afya, Elimu, Barabara nk.

Nichukue fursa hii kuwaomba Wananchi wa Kata zote za Kaliua kushiriki kikamilifu katika kukabiliana na changamoto zinazotuzunguka. Aidha, tutumie kikamilifu fursa zinazopatikana ili kuweza kujiletea maendeleo sisi wenyewe na Taifa kwa ujumla.

***MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU
IBARIKI KALIUA.***